# CLASS 5 REVISION TEST TERM 2 2021
# KISWAHILI

**Jaza pengo kwa kutumia neno sahihi.**

Mara __1__ vijana __2__ makubwa zaidi ya __3__ waliyonayo. Hupenda kutofungwa na sheria __4__ wapate kufanya mambo __5__ wapendavyo. Mtoto lazima amkubali baba na mama kwa __6__. Mzazi mwema hupenda __7__ mtoto wake __8__ kwa adabu ili kuimarisha jina __9__.

Kifo __10__ aliyekuwa __11__ wa pili wa Kenya, Mzee Daniel Arap Moi __12__ kwa mshangao mkubwa. __13__ wengi walimkumbuka __14__ mengi aliyoyafanya. Wanafunzi wa wakati wa uongozi wake walisema walipenda maziwa __15__ shuleni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mingi | B. nyingi | C. zingi | D. vingi |
| **2.** | A. hupenda | B. walipenda | C. watapenda | D. wamependa |
| **3.** | A. ile | B. pale | C. yale | D. zile |
| **4.** | A. lile | B. ile | C. hili | D. ili |
| **5.** | A. jinsi | B. vile | C. hivyo | D. hivo |
| **6.** | A. adhabu | B. adabu | C. taabu | D. tabu |
| **7.** | A. kumwona | B. kuona | C. kumuona | D. kumwonea |
| **8.** | A. akikuwa | B. akikwua | C. akikua | D. akikuua |
| **9.** | A. zake | B. kwake | C. yake | D. lake |
| **10.** | A. cha | B. la | C. ya | D. za |
| **11.** | A. rais | B. rahisi | C. raisi | D. raais |
| **12.** | A. ilitangazwa | B. kilitangaza | C. alitangazwa | D. kilitangazwa |
| **13.** | A. Wananji | B. Wananchi | C. Wanachi | D. Wanainchi |
| **14.** | A. na | B. za | C. kwa | D. ya |
| **15.** | A. aliyopewa | B. waliopewa | C. aliopewa | D. waliyopewa |

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Nomino **kazi** linapatikana katika ngeli gani?

A. U - I B. I - U

C. I - ZI D. LI - YA

17. Tarakimu **9999** kwa maneno ni

A. elfu tisini na tisa na tisini na tisa

B. elfu tisa mia tisa, tisini na tisa

C. mia tisa elfu tisa na tisini na tisa

D. tisini na tisa elfu na tisini na tisa

18. $^{1}/_{4}$ kwa Kiswahili hutamkwa

A. lopo B. lobo

C. robo D. akwota

19. **Jaza pengo kwa kutumia jibu sahihi:-**

Kifaru ____________ ni mkali.

A. yeyote B. lolote

C. chochote D. wowote

20. Mama wa baba ni

A. bavyaa B. bibi

C. wifi D. babu

21. **Andika ukubwa wa:-**

Mtoto alianguka mtihani.

A. Toto lilianguka mtihani.

B. Jitoto lilianguka jitihani.

C. Mtoto alianguka mtihani.

D. Mtihani alianguka mtoto.

22. **Tumia kivumishi kifaacho kukamilisha sentensi hii:-**

Jitu ____________ limeshikwa.

A. mwingine B. jingine

C. lingine D. kengine

23. **Jibu la kitendawili:-**

"Babu amesimama kwa mguu mmoja," ni

A. mti B. upanga

C. uyoga D. mguu mmoja

24. **Wingi wa:-**

Mama anaendа shambani ni ____________.

A. mama linaenda shambani

B. wamama wanaenda mashambani

C. akina mama wanaenda mashambani

D. wamama wanaenda akina shambani

25. **Tumia -amba- kwa usahihi:-**

Kibogoyo __________ ni mwizi alishikwa.

A. ambao B. ambaye

C. ambalo D. ambai

26. Mahali ambapo miili ya wafu huifadhiwa huitwa

A. ufuoni B. zahanati

C. kungawi D. wadi

27. **Kivumishi cha sifa ni kipi katika sentensi hii:-**

Mzee mweusi ana hasira sana.

A. Mzee B. mweusi

C. ana D. hasira sana

28. **Kanusha sentensi:-**

Mtoto amefika shuleni.

A. Mtoto hakufika shuleni.

B. Mtoto hajafika shuleni.

C. Si mtoto amefika shuleni.

D. Mtoto hawezifika shuleni.

29. Vazi gani huvaliwa na wavulana na wasichana?

A. Rinda B. Surupwenye

C. Kaptura D. Nguo

30. Kati ya maneno yafuatayo ni lipi sio salamu?

A. Mbunguni B. Salama

C. Vyema D. Chewa

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Hali yoyote ile iwayo wengi wa watoto huteswa sana. **Inatiririsha machozi** tiriri kuona mtoto malaika akinyimwa nafasi ya kwenda shule kwa ajili ya kuajiriwa. Mtoto akosapo masomo huwa ramani ya maisha yake imeanza kuchoreka vibaya. Isitoshe, mtoto huyo arundikiwa kazi ya sulubu.

Wengi hurauka jimbi la kwanza na kuanza kazi. Mtoto huyo ambaye amelala kuchelewa kwa ajili ya kazi kama vile kuosha vyombo, kupiga deki, ndiye anayetarajiwa kuamkia jikoni kutayarisha staftahi.

Zaidi ya hapo huenda alilala njaa kwa kunyimwa chakula au hata makombo.

---

**31.** Ni akina nani husumbuliwa sana?

A. Watu  B. Wazee
C. Wavulana  D. Watoto

**32.** Maneno **"inatiririsha machozi"** yana maana

A. inatoa jasho  B. inatoa makamasi
C. inahuzunisha  D. inaomboleza

**33.** Neno lingine lenye maana sawa na staftahi ni

A. kiamsha kinywa  B. chamcha
C. kazi ya asubuhi  D. kishuka

**34.** Akina nani hulala bila mlo?

A. Akina baba  B. watoto
C. watu  D. wavyele

**35.** Kazi za aina ngapi zimetajwa katika taarifa?

A. Tano  B. Nne
C. Nyingi  D. Tatu

**36.** Kazi ya sulubu ni kazi

A. rahisi  B. ndogo
C. ngumu  D. ya kuogofya

**37.** Kulingana na taarifa, mtoto anastahili

A. asome
B. ateswe
C. afanye kazi
D. achore ramani

**38.** Wengi **hurauka jimbi la kwanza** ina maana

A. kuamka asubuhi na mapema
B. kulala mapema
C. kuwa wa kwanza kuamka
D. kufanya kazi asubuhi

**39.** Makombo kulingana na taarifa hii ina maana chakula

A. kilichoharibika  B. kilicholala
C. kilichosalia  D. kilichochomwa

**40.** Kichwa cha taarifa hii ni

A. Elimu ya watoto
B. Mateso ya watoto
C. Umuhimu wa masomo
D. Ramani ya watoto

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Kwa kweli binadamu haachi kusafiri. Ziara zake kutoka mahali hadi pengine husababishwa na mambo mengi. Ama mwanadamu hutafuta chakula, hutembelea aila yake, hutafuta kazi itakayompatia riziki, hutafutia wanyama malisho na kadhalika.

Safari za hapo nyuma zilikuwa ngumu. Watu **walipiga milundi,** wakaipitia katika nyika zenye hatari kubwa lakini sio ajabu kwamba yote hayo yamepitwa na wakati. Njia za usafiri zimeimarika tangu watu waone mwangaza.

Ni dhahiri shahiri kupitia idadi ya matatu, mabasi, ndege, garimoshi, bodaboda, baiskeli na kadhalika . Na hayo yote umewawezesha kupitia uongozi bora ambao umewezesha wananchi kupiga hatua kubwa katika masomo ambao ndio ufunguo wa kila kitu.

**41.** Ni nini binadamu haachi kufanya?

A. Kuchoka B. Kutembea
C. Kucheza D. Kutafuta chakula

**42.** Usafiri unawezesha watu

A. kufahamu mengi B. kuona machache
C. kuona mwangaza D. kuona juu

**43.** ***"Kupiga milundi"*** ina maana

A. kuoga B. kupigana
C. kutembea D. kuchutama

**44.** Ni ipi si sababu ya binadamu kutembea? Kutafuta

A. chakula B. riziki
C. malisho ya wanyama D. biashara

**45.** Ziara za zamani zilikuwa ngumu kwani watu

A. walipiga milundi
B. waliuawa na wanyama pori
C. walipanda milima mirefu,
D. walivuka mito na maziwa

**46.** Vifaa hivi vyote vya usafiri vimetajwa isipokuwa

A. basi B. teksi
C. pikipiki D. matatu

**47.** Uongozi bora ni uongozi

A. mufti B. mbaya
C. mpya D. duni

**48.** Watu **waone mwangaza** ina maana

A. wawashe taa B. waerevuke
C. jua kuchomoza D. mapambazuko

**49.** Malipo anayotozwa abiria huitwa

A. kodi B. gharama
C. nauli D. faini

**50.** Taarifa hii inahusu

A. uongozi bora
B. usafiri wa nchi kavu
C. wanadamu na ziara
D. usafiri

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com